HOTUBA YA KATIBU MKUU KIONGOZI BALOZI OMBENI Y. SEFUE AKIFUNGA SHEREHE ZA MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA KATIKA VIWANJA VYA MNAZI MMOJA, DAR ES SALAAM TAREHE 23 JUNE, 2014

Ndugu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI;
Ndugu Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu Mliopo;
Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam;
Wakuu wa Taasisi za Umma;
Ndugu Washiriki wa Maonesho ya Wiki ya Utumishi Wa Umma;
Wageni Waalikwa;
Ndugu Waandishi wa Habari;
Mabibi na Mabwana,

1. Kwanza kabisa, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuruni kwa kunipa nafasi hii ya kuwa Mgeni Rasmi kwenye Kilele cha Sherehe za Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma nchini kwa Mwaka 2014. Hii ni fursa muhimu kwangu kama Mkuu wa Utumishi wa Umma, na kwa kweli napenda kupitia fursa hii, kuzungumza na Watumishi wote wa Umma. Kutokana na hali hii nachukua fursa hii kwa niaba ya Serikali, kwanza kuwapongeza Watumishi wote wa Umma kwa kuadhimisha siku hii.

2. **Ndugu Watumishi wa Umma**, Maadhimisho ya Sherehe za Wiki ya Utumishi wa Umma tunayohitimisha leo yana historia ndefu na yanaendelea kuimarika. Katika Taifa letu, Maadhimisho haya yalianza mwaka 2001, baada ya kukubaliwa katika Umoja wa Mataifa, na Umoja wa Afrika kuwa siku ya tarehe 23 Juni ya kila mwaka itambuliwe na kuadhimishwa kama siku ya Utumishi wa Umma. Maazimio haya ya kimataifa yalifikiwa baada ya kutambua mchango wa Watumishi wa Umma katika Maendeleo ya Nchi Wanachama kutokana na nafasi yao muhimu kama nguzo ya maendeleo ya Taifa lolote. Watumishi wa Umma wanayo majukumu makubwa na pia dhamana kubwa katika jamii, na ningependa kurejea maeneo machache yafuatayo:

- Kuwashauri Viongozi katika masuala ya kutunga na kutekeleza Sera za Kitaifa na Kimataifa;
- Kusimamia utekelezaji wa Sheria na kutoa haki;
- Kutoa huduma za ugani;
- Kulinda dola na kusimamia amani katika jamii;
- Kusimamia Utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo;
- Kutoa moja kwa moja huduma za kijamii kama vile matibabu, elimu; na
- kulinda Maliasili za Taifa kama vile misitu na wanayamapori katika Hifadhi za Taifa.

3. Ndugu Watumishi wa Umma, napenda kuwakumbusha kuwa madhumuni ya kutenga siku hii muhimu ni kuwawezesha Watumishi wa Umma kutafakari namna walivyotekeleza majukumu yao kwa kipindi kilichotangulia, kujadili namna ya kuongeza ubunifu katika kutoa huduma kwa umma, kujifunza mifumo mipya na kubaini changamoto zinazowakabili katika kutekeleza majukumu yao. Kwa kufanya tathmini hizi, Watumishi wa Umma hubadilishana uzoefu ili kuweza kujifunza kutokana na wale waliofanikiwa na hivyo kuleta mapinduzi katika taratibu za utendaji kazi na uendeshaji wa Serikali. Bila shaka katika Maadhimisho haya mtakuwa mmepata wasaa wa kutafakari mambo haya.

4. Ndugu Watumishi wa Umma, kutokana na umuhimu wa kufanya tafakari ya kina ya shughuli zetu, Maadhimisho ya mwaka huu pia yalikuwa na sehemu mbili. Kwanza kulikuwa na Maonesho ya Huduma zinazotelewa na Watumishi wa Umma yaliyofunguliwa tarehe 16 Juni, 2014 na Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Sehemu ya pili ilihusisha Kongamano Maalum ambapo Watumishi wa Umma walijadili masuala mbalimbali kama sehemu ya kutafakari Utendaji wa shughuli za kila siku. Katika Maonesho haya, Taasisi za Umma 86 zilishiriki kwa kuonesha shughuli wanazozifanya na kuwaelimisha wadau wao. Baadhi ya Taasisi zilikwenda mbali zaidi na kutoa huduma za papo kwa hapo kwa wateja wao. Wapo wananchi waliopimwa afya zao na wengine kupatiwa matatibu ya maradhi

yanayowasumbua. Aidha, wapo wananchi waliopata Vitambulisho vya Taifa vya Uraia. Katika maeneo mengine Watumishi wa Umma wametoa maelezo na elimu mahsusi kuhusu namna huduma zinavoweza kupatikana katika Taasisi mbalimbali. Ni imani yangu kwamba wananchi waliopata huduma hizo watakuwa wameona kuwa Serikali imepiga hatua katika mifumo yake ya kutoa huduma. Jukumu lenu kama Watumishi wa Umma, ni kuhakikisha kuwa mnaendeleza viwango hivyo katika maeneo yenu ya kazi.

5. Ndugu Watumishi wa Umma, nimeaarifiwa kuwa hata Kongamano la Wiki ya Utumishi wa Umma lilifanyika kwa mafanikio makubwa. Katika Kongamano hilo zilitolewa Hotuba Kuu mbili, ikiwa ni pamoja na ile ya Ufunguzi iliyotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia; na Hotuba Maalum (Keynote Address) iliyotolewa na Katibu Mkuu Mstaafu, Bibi. Ruth Hiyob Mollel. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa maelekezo yake mazuri kwa Watumishi wa Umma, hasusan msisitizo wake kuhusu umuhimu wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama njia ya kuleta ufanisi katika Mifumo yetu ya kutoa huduma kwa umma. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwamba sisi kama Watendaji Wakuu wa Serikali, tunalitambua na napenda kusistiza kwamba ni muhimu Taasisi zote za umma kufanya kazi kwa karibu na Wakala wa Serikali Mtandao, kwani imeundwa mahsusi kuhakikisha kuwa tunajenga uwezo wetu wa Teknolojia hiyo kwa haraka.

6. Kuhusu Hotuba Maalum iliyotolewa na Bibi. Molell, nimearifiwa kuwa ameiasa jamii kutambua kuwa ujenzi wa uchumi imara unapaswa kwenda sambamba na Utii wa Sheria. Kama nilivyosema hapo awali, ni jukumu la Watumishi wa Umma kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu. Wito wangu kwenu ni kwamba tuhakikishe kuwa tunatekeleza Sheria bila hiana, na ifikie mahali tukimwona mwenzetu anapindisha Sheria kwa makusudi, azomewe na kuondolewa katika Utumishi wa Umma, kwani atakuwa anaifedhehesha Serikali.

7. Ndugu Watumishi wa Umma, pamoja na Mada hizi muhimu, zilikuwepo nyingine ambazo nimearifiwa kuwa zililenga kutathmini ufanisi wa utoaji wa huduma, na pia Utekelezaji wa Majukumu ya Serikali. Sina shaka kuwa mada zilitolewa na watu mahiri, wataalamu waliobobea katika uendeshaji wa shughuli za Serikali, na usimamizi wa maendeleo kwa ujumla. Watoa mada hawa waliongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Mzee wetu Phillemon Lutangilo Luhanjo. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru watoa mada wote kwa kujumuika nasi katika Maadhimisho haya na kutupa utaalamu wao ambao naamini, utasaidia sana katika mipango yetu ya kubuni Sera na Taratibu zetu za uendeshaji wa shughuli za Serikali. Ni imani yangu kuwa tutajumuika nao tena mwakani katika Maadhimisho ya siku ya Utumishi wa Umma.

8. Ndugu Watumishi wa Umma, naamini kwamba kama ni tathmini ya mafanikio tumeipata. Napenda sasa niongelee changamoto zinazoukabili Utumishi wa Umma kama moja ya malengo ya Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma. Changamoto ni nyingi sana na huenda nyingine mmeziona wakati mkizungumza na Wadau wenu waliofika kwenye Mabanda ya Maonesho. Hata hivyo, Changamoto kubwa iliyo mbele yetu ni kuhakikisha kuwa tunafikia Malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (Tanzania Deveopment Vision 2025). Wote tunafahamu kuwa ipo Mipango na Mikakati iliyoandaliwa kuhakikisha kuwa malengo haya yanafikiwa kwa wakati uliopangwa. Nimearifiwa kwamba katika Kongamano nililolirejea hapo awali, kulikuwa

na Mjadala weye manufaa kuhusu namna Utumishi wa Umma unavyopaswa kujipanga kutekeleza wajibu wake wa kuweka mazingira wezeshi ili kila mdau aweze kuchangia katika kuleta maendeleo. Ni muhimu kila mmoja wenu akatambua kuwa ninyi ndio wenye dhamana hiyo ya kuhakikisha kuwa malengo yanafikiwa. Kila mtu anapaswa kujituma na kufanya kazi kwa bidii. Hayati Jonn Kenedy aliyekuwa Rais wa Marekani mwanzoni mwa miaka ya 1960, aliwahi kuwaasa wananchi wake kuwa wasiulize 'Amerika imewafanyia kitu gani', na badala yake, wajiulize "wao wameifanyia nini

Amerika". Maneno haya yana maana kubwa kwenu kama watumishi wa Umma wa Tanzania, na hivyo hata nyie, mnapaswa kujiuliza kuwa 'tumeifanyia nini Tanzania'.

9. Ndugu Watumishi wa Umma, nimelazimika kutumia maneno haya ya Hayati Kennedy kutokana na hali yetu ya kichumi ilivyo. Wananchi wetu bado ni maskini. Kama Taifa, tunakabiliwa na changamoto nyingi katika sekta za kiuchumi na kijamii;- miundombinu isiyoridhisha, Vijana wetu hawana madawati na walimu wa kutosha, maji hayapatikani kwa kiwango kinachotakiwa, na huduma duni za afya hasa kwa akina mama na watoto, bila kusahau janga la UKIMWI. Mambo yote haya yanahitaji uwekezaji wa Serikali, hali ambayo inaifanya Serikali kushindwa kuwalipa misahara ya kutosha watumishi wake. Napenda kuwaasa kuwa mtambue kuwa kwa sasa tuko kama mkulima anayeandaa na kupanda shamba ili kesho aweze kupata chakula cha kutosha. Wakati Serikali ikiwekeza katika Sekta za vipaumbele kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Muda Mrefu wa Kukuza Uchumi na Maendeleo (Tanzania Long Term Perspective Plan), ni wazi kuwa kutakuwepo umuhimu wa kuwa na uwiano kati ya uwekezaji huo, na bajeti ya malipo ya mishahara. Wakati ni kweli kuwa watumishi wa umma wanahitaji ujira mzuri, ni muhimu mkazingatia ukweli huu, japokuwa pale itakapowezekana, Serikali itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi wake.

10. Ndugu Wafanyakazi, kabla ya kumaliza hotuba yangu, ningependa niseme machache kuhusu maadhimisho haya. Kama walivyokwishatuasa wahenga wetu, ukiona vinaelea ujue vimeundwa. Bila shaka kuna watumishi wa umma ambao walitumia muda na nguvu zao kuhakikisha kuwa maadhimisho haya yanafanikiwa. Nitakuwa mnyimi wa shukrani endapo sitatambua mchango wao katika kufanikisha maadhimisho haya. Hivyo basi, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Rais, **UTUMISHI** kwa kuratibu maonesho haya. Aidha, nawapongeza watumishi wote wa umma walijitolea muda na nguvu zao kuandaa, na hatimaye kushiriki katika maadhimisho haya ambayo yatafungwa rasmi hivi punde.

11. Nawapongeza Viongozi wote ambao kwa namna moja ama nyingine waliweza kutenga muda wao na kujumuika nasi katika hatua mbalimbali za maonyesho kuanzia uzinduzi wake, kongamano na hatimaye siku ya leo yanapofikia tamati. Wametutia moyo na tunaahidi kuwa Serikali itayafanyia kazi maoni na maelekezo yao.

12. Ndugu Watumishi, napenda kuwapongeza wote waliopata tuzo za ubunifu. Ni matumaini yangu kuwa mtazitumia tuzo hizo kama chachu ya kuendelea kuboresha huduma zenu kwa wadau wenu. Kwa wale ambao hamkubahatika kupata tuzo, msikate tamaa, bali muone kama ni fursa nzuri ya kuboresha huduma zenu ili nanyi mpate tuzo katika maonesho ya miaka ijayo. Kuteleza si kuangaka.

13. **Mwisho kabisa,** nawashukuru wananchi wote waliokuja kushiriki nasi na kutupa maoni yao kuhusu namna Watumishi wa Umma wanavyowahudumia. Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali imeyapokea maoni yao, na waendelee kuuenzi Utumishi wa Umma kwa kuwa Watumishi wa Umma wapo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi. Pale watakapoona kuwa Utumishi wa Umma unatetereka, wasisite kutuarifu ili tuchukue hatua stahiki za kuurudisha mahali pake.

14. Baada ya kusema hayo, napenda sasa kutamka kwamba Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2014 yamefungwa rasmi.

NAKUSHUKURUNI SANA KWA KUNISIKILIZA